

Mkurugenzi abainisha kero sekta ya mifugo

Na Paul Mabeja, DODOMA

MKURUGENZI wa Sera na Mipango katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Amos Zephania, amesema sekta ya mifugo bado inakabiliwa na matatizo mengi yakiwamo magonjwa kwa mifugo.

Zephania aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha salamu za Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, katika ufunguzi wa kongamano la saba la wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi kuhusu sera katika sekta hizo.

Alisema sekta ya mifugo nchini bado inakabiliwa na kero nyingi

yakiwamo magonjwa ambayo yamekuwa yakiathiri kwa kiasi kikubwa mifugo nchini.

Kutokana na hali hiyo, alisema wizara inatoa wito kwa wadau mbalimbali kuwekeza katika kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa dawa za mifugo ili kukabili kero hiyo.

Aidha, alisema kero nyingine ni upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo hali ambayo imekuwa sababu kubwa inayoathiri sana sekta hiyo nchini.

"Wakati wa masika hata ng'ombe wale wa kienyeji utoaji wa maziwa unaongezeka. Lakini wakati wa kiangazi kiwango cha maziwa ki-

nashuka na hii ni kutokana na uhaba wa maji pamoja na malisho ya mifugo. Nitoe wito kwa wadau kutafuta namna ya kuzalisha malisho," alisema Zephania.

Mkurugenzi huyo alisema pia kuna haja ya kuboresha mifugo inayozalishwa nchini ili kuendana na mahitaji ya sasa.

"Ng'ombe tulio nao hivi sasa nchini ni wadogo sana hawatot maziwa ya kutosha, lakini hata nyama yao ni kidogo ambayo haiwezi kuleta ushindani katika soko, hivyo kuna haja kutafuta namna ya kuboresha mifugo hii," alisisitiza.

Kadhalika, alisema kero nyingine ni uhaba wa maofisa ugani nchini

kwa kuwa wanaohitajika ni 17,000 na waliopo ni 3,397 ambao hawakidhi mahitaji.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kutokana na uhaba wa wagani, wizara imeamua kuanzisha mfumo wa M-Kilimo ambao utawawezesha wakulima kupata taarifa mbalimbali zitakazowasaidia kupata majibu ya maswali yao.

Pia alisema kuwa ili kuboresha mazingira na kuwezesha ukuaji wa sekta ya mifugo katika mwaka wa fedha 2020/21 wizara imeendelea kupitia sheria ya mifugo ambapo kanuni mpya nne zimeandalisha na kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

MWANANCHI

MWANANCHI.CO.TZ ALHAMISI, AGOSTI 5, 2021

'Bodi ya nyama ianzishe kanzidata'

Dar es Salaam. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ameiagiza bodi ya nyama kuandaa kanzidata ya wafugaji nchini, ili kurahisisha mchakato wa kuwaunganisha kati yao na wachakataji wa nyama na benki.

Ulega alieleza hayo juzi, alipozungumza na baadhi ya wafugaji na wenye viwanda vya kuchakata nyama na wauzaji. Alisema fursa za masoko ya nyama zipo, lakini baadhi ya wafugaji bado hawajazitambua kwa sababu mbalimbali, ikiwemo kuendelea kufuga kizamani. **(Bakari Kiango)**

DC aomba serikali ifungue soko la samaki

Na PETER KATULANDA, Kagera

MKUU wa Wilaya ya Muleba, Mkoa wa Mwanza, Toba Ngumila, amelomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ifungue soko lioya la samaki la Katende, illojengwa miaka mitatu iliyopita katika kijiji cha Katende, kilichopo katika kata ya Nyakabango, wilayani humo.

Ngumila alitoa ombo hilo alipozungumza na wanakijji, alipotembelea mwalo wa kupokelea samaki wa Magarini Katende na soko hilo ililopo kando ya Ziwa Victoria.

Alisema serikali haikujenga soko hilo iowa bahati mbaya, bali ni kwasababu wavuvi wa Muleba wanatembea umbali mrefu kwenda kauza samaki Buchosa, wilayani Sengerema na Mwanza na kusababishaa kupofea kwa mapato yao.

"Tunataka watu wa Mwanza na Buchosa waje kuchukua samaki hapa, kama samaki wapo iowa wingi Muleba. Soko hili zuri la samaki liko hapa, kwanini wasiye kununua hapa, ambapo serikali ilmejenga soko la kisasa iowa gharama kubwa ya fedha za walipakodi," alisitiza.

Allombwa wizara hiyo iwaonee huruma wavuvi na wananchi wa Muleba iowa kufungua soko hilo la Katende kwa kuwa kuna mwalo unaopokea samaki kutoka Ziwa Victoria uliojengwa iowa ufadhilli wa Umoja wa Ulaya (EU) kwa thamani ya sh. 31,182,000.

"Kwa hiyo rai yangu iowa wizara husika, soko hili ambalo ilmejengwa iowa fedha za mapato ya ndani ya halimashauri zaidi ya shillingi 22.5, kianze kufanya kazii ili tuinwe uchumi wa wananchi wetu, halimashauri na taifa iowa ujumla," allombwa Ngumila.

Awali, akitoa taarifa ya ujenzi wa mwalo na soko hilo, Kaimu Ofisa Uvuvi wa Wilaya ya Muleba, Maengo Nchimani, alisema miradi hiyo ilijengwa mwaka 2018 kwa lengo la kukusanya samaki wanaokidhi viwango vya kuvaliwa kisheria.

Aliongeza kuwa lengo lingine ni kusogeza huduma karibu kwa wafanyakishara na kuwasaidia kusafirisha samaki ndani na nje ya Muleba.

Alisema mwalo wa Katende ni mionganini mwa mialo mitatu illyofadhilliwa na EU ili kupokea



Tunataka watu wa Mwanza na Buchosa waje kuchukua samaki hapa, kama samaki wapo iowa wingi Muleba, soko hili zuri la samaki liko hapa...

Mkuu wa Wilaya ya Muleba,
Mkoa wa Mwanza, Toba Ngumila.

samaki wa kwenda Ulaya kutoka katika ziwa hilo. Alitaja mialo mingine kuwa ni Sota, ulioko wilayani Ronya, Mkoa wa Mara na Kigangama, wilayani Magu, Mwanza.

Nchimani alifanua kuwa mwalo wa Katende ulijengwa kwa thamani ya sh. 31,182,000 na fedha za makusanyo ya ndani sh. 22,546,450 kupitia miradi wa DASP zilijenga soko la kufanya biashara ya samaki.

Alisema soko hilo likifunguliwa litatoa na kuongeza fursa ya ajira na biashara iowa wana Katende na Muleba kwani iowa mujibu wa takwimu za mwaka 2016, Muleba pekee Ziwa Victoria ilikuwa limetoa ajira kwa wananchi 19,000 na ziwa dogo la Burigi ililopo wilayani humo ajira 342.

Wafugaji watakiwa kunenepesha mifugo

Na Oscar Job

NAIBU Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ametoa wito kwa wafugaji wote nchini kunenepesha mifugo yao ili waweze kutumia fursa ya masoko ya nyama duniani kote.

Akizungumza mkoani Dar es Salaam na wafugaji pamoja na wazalishaji wa nyama kutoka maeneo mbalimbali nchini juzi, Ulega alisema kuna kila sababu kwa wafugaji kutumia fursa ya kuwapo masoko ya nyama duniani kujingizia kipato.

Alisema wafugaji wa Tanzania wana nafasi nzuri ya kunufaika na soko hilo kutokana na kuwa na mifugo mingi ina wanachopaswa kufanya ni kuhakikisha wanainepesha ili iweze kufikia viwango vinavyohitajika katika soko.

"Tunayo Benki ya Kili-

mo ambayo inatoa mikopo ya fedha nyingi kwa ajili ya unenepeshaji wa mifugo, kikubwa kinachohitajika kwa wafugaji ni elimu kuhusu ufugaji bora, katika hili Bodi ya Nyama mnapaswa kulismamia," alisema.

Akieleza faida ya kune nepesha mifugo, Ulega alisema ni pamoja na uwepo wa viwanda vingi vinavyochakata nyama ya mifugo hususani ng'ombe na mbuzi hivyo kuwa na soko kubwa.

"Bodi ya nyama acheni kushughulika na utoaji wa vibali peke yake, mnapaswa kwenda maeneo ya wafugaji na kuwapa elimu juu ya ufugaji bora," alisema.

Alisema bodi hiyo inapaswa kutengeneza vizuri mifumo ya unenepeshaji wa mifugo ikiwamo kutoa elimu ya kutosha kwa wafugaji waliopo maeneo yote ili lengo liweze kufikiwa.

"Rais wetu Samia Suluhu Hassan amekaribisha masoko makubwa ya nyama duniani kuja nchini kwa ajili ya kupata mifugo bora ikiwamo Saudi Arabia, ni furasa kubwa sana kama mtaitumia kikamilifu," alisema.



'Livestock sector still faces water, grazing and diseases challenges'

By **Guardian Correspondent, Dodoma**

THE Director of Policy and Planning in the Ministry of Livestock and Fisheries, Amos Zephaniah has said the country's livestock sector was still being faced with many challenges including animals' diseases, water and grazing areas.

Zephaniah made the remarks here yesterday when conveying greetings from the Livestock and Fisheries Minister at opening of the Seventh Forum for the Agriculture, Livestock and Fisheries stakeholders on the sectors' policies.

He said due to the animals' diseases challenge the ministry was calling on various stakeholders to invest in veterinary drugs factories to fight the challenge.

He cited another challenge as the availability of water and grazing areas for livestock, the situation, he said has greatly affected the sector.

"During rainy seasons, even traditional cow breeds increase their production of milk but in dry season milk production drops, all this is due to shortage of water and grazing areas, hence I appeal to stakeholders to find ways to produce animals fodder," said Zephaniah.

He said it was important to improve the livestock produced in the country to go in tandem with current needs. "The cow breeds we have in the country are small, they do not yield sufficient milk, but also even their meat is very little and cannot compete in the market, hence there is the need to improve

the breeds," he stressed.

He cited another challenge facing the sector as shortage of extension officers in the country as the current need stands at 17,000 officers, but there are only 3,397.

He said to alleviate the shortage the ministry has decided to establish the "M-Kilimo" system that will enable farmers to get various reports that would assist them to get answers to their queries.

In addition, he said in order to improve the environment and spur the development of the livestock sector in FY 2020/21, the ministry continues to review laws governing the sector whereas four new regulations have been prepared and announced in the government gazette.